# *Imani ya Waanabatisti*

Translated from

***What is an Anabaptist Christian?***

Palmer Becker, author

Mennonite Mission Network, USA, ©2008 (revised 2010)
Swahili translation (by permission) ©Joseph Bontrager, 2015

# Utangulizi

Imani ya ki-Anabatisti na jinsi Waanabatisti wanavyoamini na kuishi imekuwepo tangu mwanzo wa Ukristo. Hata leo, katika madhehebu mengi na huenda katika kila tawi, wapo waamini wenye imani inayofanana na imani ya Waanabatisti wa kwanza. Anabatisti ni namna ya kuishi Ukristo. Kama walipo Wakristo wa Anglican, Batisti, na Lutheri, hivyo wapo Wakristo wa ki-Anabatisti.

“Anabatisti” ni jina lililoundwa maana yake “wanaobatiza tena.” Jina hilo lilipewa Wakristo wa karne ya 16 walioona kwamba ubatizo wa watoto wachanga hauna faida mbele ya Mungu. Kwa hiyo hao wa kwanza wakabatizana kama watu wazima juu ya ungamo wa imani yao. Hao Wakristo wa ki-Anabatisti walikuwa watangulizi wa Wakristo Wamennonite wa leo na wengine wengi wa desturi ya Kanisa Huru.

Wakristo Wamennonite wa ki-Anabatisti wanashika imani sawa na Wakristo wengi katika madhehebu mengine. Wanaamini Mungu wa Utatu, aliye mtakatifu na mwenye neema, na wanamini wokovu kwa neema kwa njia ya toba na imani. Wanaamini kwamba Yesu alikuwa ni binadamu pia alikuwa ni Mungu, na kwamba maandiko matakatifu yalipumuliwa na Roho Mtakatifu kwa hiyo ni msingi wa imani yetu. Wanaamini uwezo wa Roho Mtakatifu na kwamba Kanisa ni mwili wa Kristo. Lakini wakati mwingine wanashika imani hizo tofauti na wengine.

Waanabatisti wanaweza kuitwa “tawi la kushoto la matengenezo ya ki-Protestant.” Walitokea wakati wa mabadiliko makubwa kijamii na kiuchumi, na walitaka kuendeleza matengenezo yaliyoanzishwa na Martin Luther, Ulrich Zwingli, na John Calvin. Tangu mwanzo, Wakristo wa ki-Anabatisti wanakaza umuhimu wa kumfuata Yesu katika maisha ya kila siku, na kushirikiana na wenzao Kristo akiwa katikati, na kushinda migogoro kwa amani. Je, unaweza kujihesabu kama Mkristo wa ki-Anabatisti?

Watengenezaji wengine walifundisha kwamba wokovu hupatikana kwa njia ya imani na kupitia neema pekee, lakini waliendelea kushika nia na fikira za Konstantino na Agostino walioishi karne za nne na tano. Wakati mwingine Wamennonite wamekaza mafundisho ya Menno Simons na Waanabatisti wa karne ya 16 tu. Kila ufufuo wa kanisa huonyesha maana ya kuwa Mkristo kwa wakati ule na katika hali ile. Lakini mwisho inatubidi turudi kwa Yesu, ambaye ni mwanzo na mwandishi wa imani yetu, ili kugundua misingi ya imani ya kweli kwa wakati wetu.

Shida kubwa ya Ukristo si kwamba madhehebu ni mengi, bali ni kwamba madhehebu yanasita kujifunza kutoka kwa madhehebu mengine. Wakristo Waanabatisti wanapaswa kujifunza kutoka kwa Wakristo wengine, kwa mfano kuhusu utawala na neema ya Mungu, na jinsi ya kushiriki katika dunia yetu. Na Wakristo wengine wanaweza kujifunza kutoka kwa Waanabatisti, kwa mfano kuhusu kumfuata Yesu katika maisha ya kila siku, na

kufafanua maandiko kwa kuweka Kristo kati, na kukubali Kristo kuwa Bwana wa maisha yote.

Mwili wa Kristo ni mmoja ila viungo vyake ni vingi. Kama kiungo kimoja kinakosa kushirikisha karama zaka na maoni yake, kinakuwa kama chumvi kilichopoteza ladha yake. Katika kitabu chake, *Differentiate or Die* (*Tofautisha au Kufa*), mwandishi Jack Trout ameandika, "Kundi lisiloweza kuleta karama tofauti na wengine, litakufa." Je, ni karama gani ambayo Wakristo Waanabatisti wanaweza kuleta, na pia kuna nini wanaweza kupokea kutoka kwa wengine?

Miradi yetu na malengo yetu hubadilika, lakini ipo misingi ya pekee ya ki-Anabatisti tangu mwanzo wake, ambayo haiwezi kubadilika. Je, misingi hiyo ya pekee ya Wakristo Waanabatisti ni ipi? Kitabu hiki kitaeleza kanuni tatu kuu. Nayo ni:

1. ***Yesu* ni kiini cha imani yetu.**
2. ***Jamii* ni kiini cha maisha yetu.**
3. ***Upatanisho* ni kiini cha kazi yetu.**

Kwa mtazamo wa ki-Anabatisti, kuwa Mkristo huunganisha hayo matatu, yaani kumwamini Yesu, na kushiriki katika jamii, pamoja na kuishi kwa upatanisho. Hayo na mengine yaliyokuwa muhimu kwa Waanabatisti katika maisha yao na hata kwa kifo chao, sasa yanakubaliwa na Wakristo wengi. Ila desturi na mafundisho mengine bado yanawakwaza au kuwatatanisha. Lakini wengine wanazidi kuona mawazo ya Waanabatisti kuwa msaada katika kumfuata Yesu kwa uaminifu katika dunia ya sasa.

Kanuni hizo tatu tunazoeleza katika kitabu hiki zilitokana na mafundisho ya Harold S Bender katika hotuba yake, *The Anabaptist Vision* (*Maono ya Ki-Anabatisti*), iliyotolewa mwaka 1943 kwa shirika la American Society of Church History. Bender alieleza jinsi anavyofafanua misingi ya Waanabatisti katika maandiko yao.

1. Ukristo ni *kuwa mwanafunzi wa Yesu*. Ni kumfuata Yesu katika maisha ya kila siku.
2. Kanisa ni kuwa *ndugu katika jamaa*. Washiriki katika kanisa wanajitoa kwa Kristo, na pia wanajitoana kila mmoja na kwa hiari yake.
3. Wafuasi wa Yesu wanashika *maadili ya upendo na kutolipiza kisasi*. Sisi jinsi tulivyobadilishwa tunatafuta kuwa wapatanishi na tunakataa kujihusisha katika ukatili na vita.

Lakini maelezo hayo matatu yalifundishwa na wengine kabla ya Waanabatisti kuyashika. Katika kitabu hiki tutaeleza jinsi mafundisho hayo yalivyotokea na kuendelezwa, na tutapendekeza jinsi yanavyoweza kufaa katika dunia ya sasa. Halafu tutayafananisha na mafundisho mengine na tutaongeza maswali ya kujadiliana. Kweli nimekaza mambo ya Waanabatisti yanayotujenga tu na sikutaja mengine yasiyofaa. Kusudi langu ni kutoa nafasi kwa wanaotaka kuuliza na kujibu swali, "Je, Mkristo wa ki-Anabatisti wa kweli yukoje?"

Watu wengi wamenitia moyo kwa kazi hiyo. Lakini maneno ya kitabu hiki ni yangu, najua ya kuwa Wakristo wengi watajikuta kwa namna mbalimbali kati ya maoni na mawazo ninayoeleza hapa.

# Kanuni ya 1. Yesu ni kiini cha imani yetu

**Yesu** alianza huduma yake mnamo mwaka 30 akikusanya kundi la wanafunzi. Kwa kipindi cha miaka mitatu wanafunzi hao waliishi, na kula, na kufanya kazi na Yesu. Waliangalia jinsi alivyowahurumia maskini, na alivyoponya waliougua ugonjwa, na alivyofanya vipofu kuona tena, alivyowasamehe wenye dhambi, na alivyowafundisha watu wote. Wakati wa huduma hizo na tena baada ya kufuka kwake, Yesu akawa katikati ya imani na maisha yao. Wakapata kumwamini kama mwalimu, na mwokozi, na bwana wao, lakini tofauti na walimu, na wokozi, na mabwana wengine wa wakati ule.

Kwa wanafunzi hao, kumfuata Yesu kulikuwa zaidi kuliko kumwamini au kumwabudu Yesu tu. Maana yake ilikuwa kujazwa Roho Mtakatifu na kumtii Yesu katika maisha ya kawaida ya kila siku. Walikuwa wamejitoa kwa Yesu na Roho Mtakatifu alikuwepo katika maisha yao. Kwa hiyo watu wakatambua kwamba walibadilishwa ili kufanana na Yesu katika mitazamo yao na jinsi walivyoishi. Ikiwa wanafunzi wa Yesu wangeulizwa, naamini wangalisema, “Yesu Kristo ndiye kiini cha imani yetu.”

Kwa miaka 250 baada ya Kristo, Wakristo waliendelea kuwa na nguvu ya Roho wa Yesu katika maisha na huduma yao. Lakini katika karne zilizofuata, mabadiliko mengi yalitokea katika imani ya Kikristo hata ilianza kuonekana kama ni dini nyingine. Watu wawili hasa wametokea kuwa wamesababisha mabadiliko hayo. Mmoja ni mwana siasa, mwingine ni mtheologia.

**Konstantino** ni kaisari wa Dola ya Rumi. Baada ya kuona maono ya msalaba mawinguni, akaacha kuwatesa Wakristo na akatangaza Ukristo kama ni dini rasmi ya Dola ya Rumi. Lakini, kuanzia utawala wake na kuendelea, Wakristo walianza kupimwa kufuatana na imani yao waliyoshika kuliko maisha yao walivyoishi.

**Agostino**, mtheologia, alitokea baada ya Konstantino. Aliongoka kwa namna ya ajabu na wengine wamemwita mtheologia mkuu wa Kanisa la Magharibi. Lakini kidogo maono na mabadiliko yalitokea tofauti na wanafunzi wa kwanza. Badala ya kukaza maisha na huduma ya Yesu, Kanisa lilianza kutia mkazo zaidi katika kifo chake Yesu. Imani ya Mitume, iliyoandikwa wakati huo, haitaji mafundisho na kazi ya Yesu. Badala ya kusema “*Yesu* ni msingi wa imani,” wafuasi wa Agostini walipenda kusema, “*Kifo cha Yesu* ni msingi wa imani yetu.”

Mabadiliko makubwa yalitokea. Wakristo wa kwanza waliteswa na kujikusanya kuabudu kisiri, sasa walikutana katika makanisa makubwa. Walioamini wakati wa kanisa la kwanza walifundishwa halafu kubatizwa kama watu wazima juu ya imani yao, na kujiunga na

ushirika wa waaminio. Sasa waliwabatiza watoto wachanga, na walihesabu raia wote isipokuwa Wayahudi kuwa ni washiriki katika kanisa lililojijunga na serikali wa nchi. Wakati kanisa la kwanza lilielekeza washiriki kumfuata Yesu, sasa lilikaza mafundisho na matendo ya ibada, na kujilinda na maadui yao. Wakristo wa kwanza walishuhudia imani yao kwa majirani, sasa uinjilisti ni kupanua mipaka ya "Dola ya Kikristo." Na kati ya Wakristo wa kwanza wengi walikataa kuingia jeshini, wakati wa kifo cha Agostino walikuwa ni Wakristo tu waliruhusiwa kuingia katika jeshi la Kirumi.

Kati ya miaka 1200 na 1500 baada ya Kristo, kulikuwa na watu na vikundi mbalimbali walianza kutambua kwamba kanisa lilikuwa limeachana na mafundisho juu ya wokovu na kanisa jinsi yalivyofundishwa na kanisa la kwanza. Kati ya hao watengenezaji, alikuwa mtawa wa kijerumani, aliitwa **Martin Luther**, aliyekuwa amesomeshwa theologia na maoni ya Agostino. Wengine walikuwa Ulrich Zwingli, mchungaji wa Kiswisi, na John Calvin. Hao wanateolojia walitokeza mabadiliko makubwa.

Luther hasa alikwazwa na desturi na matendo ya makuhani na mapapa kwa jinsi walivyotoa msamaha na ukombozi kutoka purgatori kufuatana na matendo ya watu, na waliuza vyeti vya msamaha. Tarehe 31 Oktoba, 1517, Luther aliweka maoni yake katika maneno 95 aliyopiga kwa msumali mlangoni mwa kanisa kuu hapo Wittenberg, Ujerumani. Tendo hilo lilianzisha matengenezo ya ki-Protestant.

Luther na Zwingli walikubali kuwa maandiko pekee yana mamlaka kuhusu imani na maisha, na wakasisitiza kwamba wokovu ni kwa neema kupitia imani tu. Lakini, wokovu huo ulieleweka kuwa na kusudi la kuleta uzima wa milele. Wengine wanauita wokovu wa roho badala ya wokovu kamili. Walifundisha kwamba Wakristo wanapaswa kumtumikia Mungu na majirani, lakini hawakukaza umuhimu wa kumfuata Yesu katika maisha ya kila siku na ushirikiano na Wakristo wenzao.

Wanafunzi wachache wa Ulrich Zwingli, wakiwemo Conrad Grebel, Feliz Manz, na George Blaurock, waliishi mji wa Zurich, Uswisi, na walikutana kila wakati kwa kuisoma Biblia. Wakati huo huo, wengine katika nchi za Ujerumani wa Kusini na Moravia, kama Hans Hut, Hans Denk, Pilgram Marpeck, na Jakob Hutter walikuwa wanatafuta mafundisho ya Biblia kuhusu maswali ya wokovu. Baadaye akatokea **Menno Simons**, aliyekuwa ametoka katika ukuhani wa Kirumi, naye akafundisha na kukusanya vikundi vya waamini waliotokea nchi ya Uholanzi.

Hao wanafunzi wa Biblia waliendelea kusoma juu ya Yesu na wanafunzi wake. Neno kuu kwa wengi lilikuwa Waebrania 12:2, "Tumtazame Yesu aliyeanzisha na anayekamilisha imani yetu." Neno kuu kwa Menno Simons lilikuwa 1 Wakorintho 3:11, "Kwa maana hakuna mtu anayeweza kuweka msingi mwingine isipokuwa ule uliokwisha jengwa, ambao ni Yesu Kristo." Pamoja na maneno hayo, waliona kwamba mwenendo wa kikristo jinsi unavyoelezwa katika Hotuba ya Yesu Mlimani (Matayo 5-7) ni maisha ya kawaida kwa Mkristo, anayeishi kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Wakristo wa kwanza wa Ki-Anabatisti walikubali Imani ya Mitume na mengi katika mahubiri ya Luther na Zwingli, lakini walidai kwamba mafundisho yao yanapungua imani ya kibiblia. Kwa fundisho la "kuhesabiwa haki kwa imani" (Warumi 5:1) waliongeza "kuzaliwa mara ya pili" (Yohana 3:3). Walikubali kwamba wokovu ni kwa neema ya Mungu, lakini walikaza umuhimu wa utii kwa upande wa waamini. Walisisitiza kwamba wokovu kupitia Yesu na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, lazima utabadilisha maisha ya mtu, ki-maadili, na ki-mahusiano, na ki-uchumi. Ubatizo wa watu wazima ulieleweka kuwa ni ishara ya wokovu huu na kuonyesha kwamba maisha ya mtu yamebadilishwa. Kama ungaliuliza hao Wakristo Waanabatisti wa kwanza, wangalijiunga na wanafunza wa kwanza wa Yesu kwa kusema, *"Yesu ndiye kiini cha imani yetu!"*

Je, neno hili latuhusu sisi leo kwa vipi? Wakristo wa ki-Anabatisti wanaelewa Yesu ni kiini cha imani yao kwa njia hizi tatu:

## 1. Tunamfuata Yesu katika maisha yetu ya kila siku

Ukristo ni nini? Ni kujisikia kuwa ni karibu na Mungu, au kukubali mafundisho fulani, au kuhesabiwa haki mbele ya Mungu? Hayo yote ni sawa, lakini zaidi ya hayo, maana ya kuwa Mkristo ni kumfuata Yesu katika maisha ya kila siku. Wakristo wa Ki-Anabatisti wanasema kuwa, "Ukristo ni Uanafunzi!" Neno la kijerumani ni *Nachfolge Christi* au "kumfuata Kristo." Kati ya Waanabatisti wa kwanza alikuwa ni Hans Denk, aliyesema, "Mtu hawezi kumjua Kristo kweli isipokuwa anamfuata katika maisha yake ya kila siku; na mtu hawezi kumfuata Kristo katika maisha yake ya kila siku isipokuwa anamjua kweli."

Maana ya wokovu kwa desturi ya Waanabatisti ni kubadilishwa kutoka maisha ya zamani hata kwa maisha yanayoonyesha nia na matendo ya Yesu. Wokovu si badiliko tu katika jinsi Mungu anavyotuona. Pia ni badiliko katika nia na matendo yetu mbele ya Mungu, na kwa watu, na mbele ya dunia. Badiliko hilo linawezeshwa na Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu, na anayewezesha wanafunzi kumfuata Yesus katika maisha yao ya kila siku.

Wakristo wengi hata baada ya kupokea wokovu wanaendelea kudhani kwamba wapaswa kufanya dhambi na wanashindwa kuishi katika ushindi na maisha mapya. Wengine wanasema, "Maisha yangu si tofauti, nimesamehewa tu." Lakini Wakristo wa ki-Anabatisti hawakubali. Wanaamini ya kwamba mafundisho na Roho wa Yesu anawawezesha kubadilishwa na kushinda nguvu za maovu. Wametiwa moyo kumfuata Yesu katika mambo yote ya maisha yao ya kila siku.

## 2. Tunafafanua Biblia kwa kuweka Kristo kwanza

Wakristo wengi wanasoma Biblia wakiona mamlaka ya sehemu zote ni sawa. Yaani kwa mfano maneno ya Mungu kwa Musa katika Agano la Kale yanabeba mamlaka kwetu sawa na maneno ya Yesu katika Agano Jipya. Kama mtu anatafuta ukweli kuhusu mambo ya kisiasa au kijamii kama vita au adhabu ya kifo, anayeamini usawa wa Biblia atasoma Agano la Kale na kufuata mafundisho yake, hata kama Yesus alifundisha mengine.

Wakristo wengine wanafafanua Biblia wakiamini kwamba Mungu alijifunua kwa njia tofauti katika vipindi mbalimbali. Ili waweze kuelewa mapenzi ya Mungu, inawabidi kwanza kujua ni katika kipindi gani neno hilo lilitamka. Hivyo, wanaamini kuwa mafundisho ya Yesu alivyofundisha katika Hotuba Mlimani (Matayo 5-7) ni kwa kipindi cha baadaye katika Ufalme wa Kristo atakaporudi duniani. Na kwa wakati huu, wanaamini kuwa Yesu hupokea sifa na ibada yetu, lakini si utii wetu.

Wakristo wa ki-Anabatisti wanafafanua Biblia yote kwa kuweka Kristo kwanza. Yesu ni ufunuo kamili wa Mungu ya mapenzi yake Mungu, kwa hiyo wakati mwingine mafundisho ya Yesu yanazidi mafundisho mengine yaliyotangulia. Yesu mwenyewe alisema, "Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, … bali mimi nawaambieni …" (Mathayo 5:21, 27, 31, 38, 43). Vivyo hivyo, mwandishi wa Waraka kwa Waebrania aliandika, "Mungu, ambaye amesema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, …. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake…." (Waebrania 1:1-3). Mmishenari Peter Kehler alisema, "Kama Biblia inanionyesha Yesu Kristo tu, imenitosha!"

Wakristo wa ki-Anabatisti wanakubali ya kwamba Maandiko yote yanatoka kwa Mungu, lakini hawafuati maneno yote kama ni maagizo tu. Biblia ni neno la maandishi, na pia kuna Roho wa Yesu, na tunahesabu yote kuwa na mamlaka. Tunafafanua Biblia kupitia Roho wa Yesu. Wanafunzi wa Yesu wanakosea ikiwa wanainua neno la maandishi juu ya Roho, au wakiinua Roho juu ya neno la maandishi. Neno na Roho lazima kushikamana.

Kwa hiyo, Wakristo wa nia ya ki-Anabatisti wanaelewa Maandiko kwamba yanatoa maarifa kuhusu Mungu, lakini wanamwelewa Yesu kama mamlaka ya mwisho kuhusu imani na maisha. Yesu ni Bwana wa Maandiko na kielelezo cha maadili ya mtu binafsi na ya kijamii. Maandishi yote mengine hayana mamlaka isipokuwa yanalingana na mafundisho ya Yesu na Roho wa Yesu. Kwa hiyo, kama Mkristo wa nia ya ki-Anabatisti atakabiliwa na swali kuhusu mambo ya mwenendo bora, watatafuta mwongozo kwanza katika mafundisho ya Yesu, ndipo watasoma maandiko mengine ili kuelewa zaidi. Na ikiwa sehemu mbili za Biblia zinaonekana kufundisha tofauti, wataweka neno la Yesu mbele.

### 3. Tunamkubali Yesu kuwa Mwokozi pamoja na Bwana wetu

Wakristo wengi wanamkubali Yesu kuwa ni Mwokozi wao binafsi kutoka dhambi, lakini hawaoni umuhimu wa kumfuata katika maisha yao ya kila siku. Wanamtazamia Yesu kuwaokoa kutoka katika mazoea yao mabaya, lakini wakati wanapokabiliwa na matatizo ya kijamii au kisiasa, wanatii mwajiri wao, au balozi, au mkuu wa jeshi, au rais. Kwa hiyo Wakristo wengi leo wanatii amri za viongozi wa kidunia kuliko amri alizotoa Yesu.

Wakristo wa nia ya ki-Anabatisti wanaamini kwamba tunapaswa kutii serikali kiasi inavyolingana na mafundisho ya Yesu. Kusudi la serikali ni kutunza uhai na taratibu katika dunia. Lakini si kama tunatii sheria zote za serikali. Utii wetu wa kwanza ni kwa

Yesu na kwa ufalme wa Mungu, kwa hiyo inawezekana tutapaswa kutotii sheria ikiwa ni kinyume cha mafundisho na nia ya Yesu. Ikiwa magongano kati ya njia ya Yesu na njia za Kaisari, tunaunga jibu la wanafunzi wa kwanza, "Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu" (Matendo 5:29).

Kwa hiyo, Wakristo wenye nia ya ki-Anabatisti ni *watu wa imani* wanaotafuta:

1. Kumfuata Yesu katika maisha yao ya kila siku.
2. Kufafanua Biblia katika Roho wa Yesu.
3. Kumtii Yesu Kristo juu ya mamlaka nyingine zote.

*Yesu Kristo ndiye kiini cha imani yao*. Je, wewe ni Mkristo wa ki-Anabatisti?

# Kanuni ya 2. Jamii ni kiini cha maisha yetu

Mwanzo wa kazi yake Yesu aliunda jamii ya wanafunzi. Alimkaribisha Petro na Andrea halafu Yakobo na Yohana kujiunga naye. Baada ya si muda mrefu walikuwa wengi waliomfuata na kati ya hao aliwachagua wanafunzi 12 (Marko 3:13-19). Wakajifunza, walikula, walisafari, na kuhudumia pamoja hadi hapo siku ya Pentekoste walikuwa kiini cha jamii mpya iitwayo kanisa. Katika Matendo 2 waamini wa kwanza walikutana siku kwa siku, si katika hekalu tu, bali pia "wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote" (Matendo 2:46).

Kanisa katika Agano Jipya lilionyesha maisha yaliyokuwa tofauti na desturi za kidini na kisiasa za siku hizo. Maisha hayo tofauti waliyafundisha na kuyafurahia katika eneo la hekalu, pia katika vikundi vyao nyumbani.

Yesu alieleza hali ya kanisa kwa kutumia mfano wa jamaa. Hivyo ilikuwa wazi kwamba Yesu alitaka wanafunzi wasimwamini tu, bali kushirikiana katika hali ya undugu kama katika jamaa moja. Watu walipotazama jinsi Mungu alivyowafanyia katika makundi hayo na kupitia makundi hayo, wakashangaa. Wanafunzi walikuwa na karama, na nia, na ujasiri kuendeleza kazi ya Yesu alivyofanya alipokuwa nao kimwili. Kama ungaliwauliza hao wanafunzi wa kwanza wa Yesu, wangalikujibu, *Jamii ya kikristo ni kiini cha maisha yetu!*

Lakini mfalme **Konstantino** badala ya kukaza hali ya kanisa inayofanana na jamaa ya ndugu na dada waliokutana na kusoma Biblia, alikaza kwamba kanisa ni kundi linalokutana katika makanisa makubwa. Watajiri ambao walikuwa wamepinga maisha ya wokovu, sasa walikuwa tayari kujiunga na kanisa lililohusika na mfalme. Watu wengi walibatizwa hata wasiokuwa wanamfuata Yesu kweli. Kufuatana na hali hiyo, badala ya kanisa duniani, ile "dunia" iliingia ndani ya kanisa.

Kwa msaada wa mama yake na kutiwa moyo naye, Konstantino alianza kujenga makanisa makubwa huko Rumi na pia mahali alipozaliwa na alipokufa Yesu. Haikuchukua muda

mrefu makanisa yalijengwa katika karibu kila mji. Badala ya kusema, “jamii ya kikristo ni kiini cha maisha yetu,” Wakristo walianza kusema, “jengo la kanisa ni kiini cha mji wetu.”

Mtheologia **Agostino** alijitahidi kuwa mtiifu katika maisha yake ya binafsi, kati ya watu waliohesabu kwamba watu wote ni Wakristo. Yeye na wanafunzi wake waliona kwamba haiwezekani kutofautisha wale waliojiunga na mwili wa Kristo na wengine wasiojiunga. Alisema, “lazima ngano na magugu kukomaa pamoja.”

Badala ya kutambua Kristo katika jamii ya waaminio, Agostino alikaza kuwa tunatambua Mungu katika matendo ya ibada. Imani iliyotokea ni kwamba msamaha wa dhambi ya asili hupatikana katika ubatizo. Na msamaha wa dhambi za kila siku hupatikana katika misa (Meza ya Bwana). Karne zilizofuata ilitokea imani katika purgatory, na kwamba mtu ataweza kutoka katika purgatory mapema kwa njia ya kuombea watakatifu, na kutoa sadaka kwa maskini, na kununua msamaha kutoka kwa papa.

Kufuatana na hayo, imani ya kwamba Wakristo wameunganishwa na Kristo na pia kwa Wakristo wenzao, ilianza kupotea. Waliotaka kumfuata na kumtii Yesu na kujiunga na jamii ya kikristo waliamua kuwa watawa na walikaa katika nyumba wakitengwa na watu wa kawaida. Ilianza kuonekana kwamba haiwezekani mtu wa kawaida kumfuata Yesu katika maisha ya kila siku na kuishi katika jamii ya kikristo.

**Martin Luther** na watengenezaji wengine walitaka mwanzoni kutengeneza kanisa kwa kufuata mafundisho ya Biblia. Wakajitenga na kanisa la Rumi na katika mahubiri yao walikaza ukuhani ya waaminio wote. Ila wengi waliowafuata Luther na Zwingli walikuwa wakulima waliotaka kujiweka huru na utawala wa mabwana na watawala waliowatesa wa wakati ule. Wakulima wengine walianza kushika silaha ili kuwashinda wakubwa hao, na Luther na Zwingli walitaka kulinda usalama na wakatetea wakubwa wa serikali. Na kwa njia hiyo, bila kutaka, walianzisha mapatano mapya kati ya kanisa na serikali. Kwa njiia hiyo, walikwaza wakulima wengi wasiwaamini.

Ilitokea Vita ya Wakulima na hivyo Luther na Zwingli hawakufaulu kutekeleza matengenezo makuu jinsi walivyotaka. Wakaendelea kufuata taratibu za Konstantino na theologia ya Agostino, wakakubali kanisa liwe kanisa la serikali. Ubatizo wa watoto wachanga ulikuwa mlango wa kuingia katika ushirika wa kanisa, upanga wa serikali ulitumiwa kama chombo cha kutunza taratibu, na waliona kwamba sehemu zote za Biblia, yaani Agano la Kale na Agano Jipya, zinafafanua mapenzi ya Mungu kwa usawa.

Waanabatisti wa kwanza, na Menno Simons naye, walisikitikia jinsi Matengenezo hayakutimilika. Hawakutaka kulirudisha kanisa kwa taratibu zile tu zilizoanzishwa na Konstantino na Agostino. Walitaka kulirudisha kanisa kwa hali yake lilivyokuwa katika Agano Jipya. Waliamini kwamba inapasa kanisa kuwa tofauti na kutengwa na taratibu za dunia.

Kwa sababu ya mateso, ilibidi Waanabatisti wa kwanza kukutana kwa siri ili kusoma Biblia, kushirikiana, na kwa maombi na ibada. Katika nyumba zao na katika mahali pa

kujificha mara nyingi walimpokea Kristo kati yao. Walioanza kumwamini Yesu Kristo na wakaahidi kumfuata katika maisha ya kila siku, wakabatizwa na kupokelewa katika kundi la waamini kama mshiriki pamoja nao.

Vikundi hivyo walitoa ushuhuda wa nguvu katika mikoa yao. Msomi kutoka nchi ya Japan, Mchungaji Takashi Yamada, alisoma maandiko ya wasomi wengine 62 waliochunguza mwanzo wa Waanabatisti. Akatambua kwamba "katika kanisa la asili pia kati ya Waanabatisti wa kwanza, jambo la kipekee ni kwamba walikutana katika vikundi walipozea kuonyana na kutiana nguvu na hivyo kuwawezesha kushuhudia mbele ya dunia."

Wakristo wa ki-Anabatisti walizoea kutaja nguvu ya kuishi maisha yaliyo tofauti na taratibu za dunia. Walidai "maisha matakatifu" kutoka kwa washiriki wote wenzao, na hasa kutoka kwa viongozi. Walieleza kwamba Mkristo mwaminifu ni yule anayeishi kwa uongozi na taratibu za Roho Mtakatifu, wala si yule ambaye amesamehewa dhambi zake tu. Na walioacha kumfuata Yesu katika maisha yao ya kila siku au kuendelea kwa namna isiyofuata namna ya ki-Kristo wakatengwa na mwili wa Kristo.

Waanabatisti waliamini kuwa kanisa ni waamini waliobadilishwa na waliokuwa wamejitoa kwa Yesu na wameahidi kutembea pamoja katika ushirikano. Lakini makanisa mengine, ya ki-Protestanti pamoja na ki-Katoliki, wakaona hayo kuwa ni tishio kwa makanisa yao. Kwa hiyo wakawafunga na kuwatesa Waanabatisti wengi. Waliokufa kwa kuzamishwa majini, au kukatwa kichwa, au kuchomwa motoni kwa ajili ya imani yao, walizidi 4,000.

Kati ya Waanabatisti wa kwanza zilikuwepo na tofauti nyingi. Wengine walikaza zaidi mambo ya mwisho wa dunia. Wengine walianza kuvuruga na kutumia nguvu za kidunia. Kwa mfano, katika mji wa Munster, Ujerumani, kundi moja lilichagua wazee 12 na kuwaweka badala halmashauri ya mji na wakajitangaza kuwa Israeli Mpya. Nao walianza kuongeza wake na kushika silaha za serikali kujilinda. Matendo ya kundi hili la pembeni yaliharibu sifa za Wakristo wa ki-Anabatisti na ki-Menno, na kuna wengine wanaoamini sifa hizo mbaya hata leo.

Kwa imani yao ya kwamba ni watu wa Yesu, na jinsi walivyosaidiana, Waanabatisti wa kwanza walipata uwezo wa kuwa waaminifu katika dunia iliyowapinga. Kama ungaliwauliza, naamini wangalikujibu pamoja na wanafunzi wa kwanza wa Yesu, "Kiini cha maisha yetu ni jamii ambayo imeweka Kristo kwanza."

Katika dunia ya leo, sisi Wakristo wa ki-Anabatisti wanaelewa kwamba jamii ni kiini cha maisha yetu kwa njia hizi tatu:

**1. Msamaha ni lazima katika jamii**

Yesu alikuja ili tuwe na uzima na tuwe nao tele. Akaomba kwa nguvu kwamba, jinsi yeye ni mmoja na Baba yake, vivyo na sisi tuwe na umoja kati yetu. Kwa hiyo, ikiwa sisi mwili

wa Kristo tunakubali kuombeana msamaha, tunajenga umoja wa karibu pamoja na faida zake. Toba na msamaha zinaondoa vizuizi vinavyozuia ushirikiano wetu na Mungu na kati mwetu. Wakristo wa ki-Anabatisti wanaamini kwamba msamaha ni lazima ili kujenga na kutunza ushirikiano.

Tatizo la kimsingi kati ya wanadamu si kukosa pesa, kukosa elimu, wala kukosa uwezo. Tatizo la kimsingi ni kwamba tunakoseana. Tangu mwanzo sisi binadamu, tukiwa binafsi au katika vikundi, tumemkosea Mungu na wenzetu katika mawazo na matendo yetu. Matokeo ni kuvunja mahusiano na Mungu, na wenzetu, hata na roho yetu ndani yetu, na ulimwengu mzima.

Upatanisho huwezekana iwapo upande mmoja hutubu kweli na kuomba msamaha. Lakini kwa bahati mbaya katika dunia pasipo nia ya kikristo mwanadamu hujaribu kusahau bila msamaha. Mara nyingi tunakataa matendo yetu na kujitetea badala ya kutubu kweli na kusamehe.

## 2. Biblia hufafanuliwa katika jamii

Wakristo wengi wanaposoma na kuchunguza Biblia baadaye wanatangaza yale waliyoelewa wenyewe kama ni ukweli kamili. Na huwa kama mtu anategemea tu ufafanuzi wake binafsi ananza kuelewa na kueleza mambo ya makosa na ya kubabaisha.

Wakristo wengine wanaamini kwamba ni wachungaji, na makuhani, na walimu tu wanaoweza kuelewa na kueleza Maandiko kwa ukweli. Kwa hiyo wengine wanaacha kusoma Biblia na kutafuta maana yake.

Wakristo wa nia ya ki-Anabatisti huamini kwamba ili kufafanua Biblia vizuri, inambidi kila mtu binafsi kusoma Maandiko halafu kushauriana katika kundi la waamini. Na hayo yote kwa uongozi wa Roho Mtakatifu. Ni kawaida tukijikusanya katika vikundi, madarasa, na mikutano na tukiongozwa na Roho wa Kristo, tunaweza kujua maana ya Maandiko na kutatua maswali yanayotukabili.

## 3. Jamii ni kukutana uso kwa uso

Kanisa linafanana na ndege yenye mabawa mawili. Bawa moja ni jamii kubwa likiabudu, tunakaza uhusiano wetu na Mungu Mtakatifu anayezidi akili zetu. Bawa la pili ni vikundi vidogo tunapokaza uhusiano wetu wa karibu na uso kwa uso. Ndege kuruka huhitaji mabawa yote mawili.

Mahusiano ya maana huwa ni katika vikundi vidogo vya watu wasiozidi 12. Tumeona hayo wakati tukikutana kwa kushauriana, au kutambua vipawa vyetu vya huduma, au tukijikusanya kwa kushirikiana tu. Makanisa yenye uzima huweka taratibu za kuwezesha ushirikiano. Mara nyingi ni ushirika wa vikundi. Wengine wanasisitiza kwamba vikundi ni asili ya kanisa.

Kujumlisha, Wakristo wa nia ya ki-Anabatisti wanazoea jamii ya kikristo kama kiini cha maisha yao. Wanaona kwamba:

1. Msamaha ni lazima kwa ushirikiano.
2. Maongezi na kushauriana ni lazima katika kufafanua Maandiko.
3. Vikundi vidogo vikikutana uso kwa uso ni jambo la kimsingi katika uzima wa kanisa.

*Kumwamini* Yesu, *kushiriki* katika kanisa, na *kutenda* matendo mapya hujenga jamii ya kikristo.

Je, wewe ni Mkristo wa nia ya ki-Anabatisti?

# Kanuni ya 3. Upatanisho ni kiini cha kazi yetu

Mungu alituma mwanaye, **Yesu**, ili afumbue tatizo la dhambi. Yesu alikuja kutupatanisha na Mungu na pia kutupatanisha na wenzetu. Yesu aliona hali ya kuvunjika na udhalimu za aina zote. Na aliandaa na kufundisha wanafunzi wawe mashahidi wake na kuleta upatanisho.

Yesu alieleza hatua za kupatana katika ushirika wa imani katika Matayo 18:15-20. Mtu na watu waliokwazwa wakutane kwanza moja moja kwa kutafuta upatanisho katika tatizo linalowakwaza. Ikiwa hatua hii inashindikana hatua nyingine ni kuhusisha washiriki wengine katika kutafuta amani.

Katika Hotuba Mlimani, Yesu alifundisha wanafunzi wake kwamba amani na haki kati ya watu hutokana na kutafuta kwanza ufalme wa Mungu, na kutubu makosa, na kuwafanyia wengine kama sisi wenyewe tunataka kufanyiwa. Yesu alisema, “Msiwapende tu wanaowapenda. Hata watu wa mataifa wanafanya hivyo. Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi” (Matayo 5:43-48). Yesu hakusema bure, alisema kwa ajili yetu. Kumfuata Yesu ni *kutenda* matendo mapya.

Mwisho wa maisha yake duniani, Yesu alisema, “Kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi” (Yohana 20:21). “Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi” (Matayo 28:18-20). Baadaye wanafunzi wa kwanza walitoka na kuenea katika dunia yote iliyojulikana kwa wakati ule. Walihubiri na kufundisha, na kuishi kwa njia mpya ili watu wote wapate kupatanishwa na Mungu na watu wenzao.

Changamoto kubwa iliyowakabili Wakristo wa kwanza ilikuwa migogoro ya kikabila, na kidini, na kimila kati ya Wayahudi na Mataifa. Na mitume walipoona jinsi watu wa desturi mbalimbali waljazwa Roho Mtakatifu na kupatanishwa katika jamaa ya Mungu, walikubali ya kwamba ni kupitia imani katika Kristo tu, wala si sheria na taratibu za dini, watu wa desturi mbalimbali wanaweza kuwa mwili mmoja na kuishi kwa amani.

Karne za kwanza baada ya Yesu, waliomfuata Yesu walikataa kushika silaha za kijeshi na kuiingia katika vita. Walielewa kwamba walikuwa wamepewa amri ya kuwapenda adui zao, wala si kuwaua. “Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho,” alisema Paulo katika 2 Wakorintho 5:18. Ungaliwauliza Wakristo wa kwanza, naamini wangalijibu, *“Kupatanisha watu kwa Mungu na kwa binadamu wenzao ni kiini cha kazi yetu!”*

**Konstantino** alipoanza kuunganisha kanisa na serikali, mabadiliko makuu yalitokea katika kanisa. Yesu alisema, “Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu” (Yohana 18:36), lakini Konstantino alikuwa ni mfalme. Baada ya muda kupita, ufalme wa hiari alipotawala Yesu, yaani kanisa, ulianza kufanana na ufalme alipotawala kaisari. Imani ya Wakristo wa kwanza waliokuwa wameshika kwa nguvu ilidhoofika. Katika kanisa walikuwapo watajiri na wengine walizidi kuwa maskini. Wakristo walianza kutesa wenzao. Waliokuwa watu kutetea amani sasa waliingia vitani. Badala ya kutumia nguvu zao kwa uinjilisti, upatanisho, na kuwahudumia wengine, walitumia kiasi kikubwa cha mali yao kwa kujenga makanisa makuu katika kila mkoa wa Ulaya. Kujenga makanisa makuu ulikuwa kiini cha kazi yao.

**Agostino** alijitahidi sana kuhusu dhambi za kibinafsi kama ulevi, tamaa, michezo wa kamari, na uasherati. Lakini mafundisho na matendo yake kuhusu amani na haki yalikuwa dhaifu kwa sababu kanisa liliunganishwa na serikali ya dola. Badala ya kutafuta kupatanishwa na adui, Agostino alipata kuamini kwamba imani ya kikristo yahitaji kujilinda na adui. Alifundisha kwamba kuna “vita ya haki” inayowaruhusu Wakristo kuingia katika vita na kutumia nguvu, ili kulinda haki. Mawazo hayo kuhusu vita yanashikwa na Wakristo wengi hata leo.

**Luther**, **Zwingli**, na **Calvin** walifanya mengi mazuri. Luther aliunda mpango wa “mfuko wa jamii,” na Calvin alijaribu kuweka taratibu za kikristo katika maisha. Lakini, kama Agostino, walikaza msamaha wa kibinafsi, na kutii kwa Amri 10 za Mungu, lakini mafundisho na mwenendo yalikuwa dhaifu, juu ya neema inayobadilisha maisha, na uinjilisti, na upatanisho.

Wakristo wa kwanza wa ki-Anabatisti chini ya uongozi wa **Menno Simons** na wengine walijitahidi kuelewa na kufundisha namna ya kuishi kama mwili wa Kristo duniani. Waliamini kwamba wafuasi wa Yesu wanaweza kufanana na Yesu na *kutenda* kama Yesu alivyotenda, kwa kazi ya Roho Mtakatifu, na kwa kuahidiana kujiunga pamoja.

Waanabatisti wa kwanza walikutana katika nyumba zao na katika vikundi. Hapo walitambua uwepo wa Roho Mtakatifu. Walichunguza Maandiko kama msingi wa maisha yao na kushauriana jinsi ya kuishi kikristo. Waanabatisti waliona Maandiko kuwa ni “silaha” yao pekee. Katika mafundisho yao walikaza ushirikiano kiuchumi, wawe na amani na Mungu, na amani kati yao, na amani na maadui yao.

Kutokea kwa Waanabatisti kunaweza kueleweka kuwa ni uamsho wa kiroho wa wakati wa Matengenezo. Viongozi wao walifundisha kuhusu nguvu za Roho Mtakatifu kuliko watengenezaji wengine. Waliamini kwamba ni Roho Mtakatifu anayewawezesha kwa maisha ya kumfuata Yesu, na kufanya uinjilisti, na kwa huduma ya upatanisho, na kuishi maisha ya kiroho.

Waanabatisti pia walikuwa wainjilisti hodari wa karne la 16. Viongozi wao walidumu katika kutembelea sehemu zote za Ulaya wakijaribu kupatanisha watu kwa Mungu na kwa wenzao. Maelfu ya watu waliingia katika uhusiano na Yesu na wakajiunga na shirika za ki-Anabatisti. Shirika hizo zilitokea na kuenea katika sehemu nyingi za Ulaya.

Pamoja na hayo, Waanabatisti walisaidia kuendeleza haki katika jamii. Vikundi vingi vya ki-Anabatisti vilijulikana kwa ajili ya jinsi walivyoshirikiana kiuchumi na pia kwa jinsi walivyotafuta kuleta haki kwa watu wote. Wakulima wengi walikuwa wanaupinga utawala mkali wa mabwana wao, na viongozi na waamini wa ki-Anabatisti walijaribu kuleta matatizo hayo mbele ya watawala. Katika vikundi vyao waliunda jamii iliyokuwa badala ya jamii ya dola au ya mabwana. Waliona haiwezekani mtu anayemfuata Yesu kweli na aliyebadilishwa na Roho wa Mungu na kubatizwa katika mwili mmoja wa Kristo, kunyima mali na vifaa yake kwa ndugu anayeishi katika shida.

Jinsi walivyoelewa Maandiko na jinsi walivyoahidiana kumfuata Yesu katika maisha ya kila siku, Wakristo wa ki-Anabatisti waliamini kwamba kushiriki katika vita ni kosa. Sawa na wanafunzi wa kwanza, walikataa kujiunga na jeshi hata kama Waturuki wa ki-Islamu walikuwa wanavamia Ulaya. Badala ya kupigana juu ya maadui, Waanabatisti walikubali kuufuata mfano wa Yesu, ambaye “alipotukanywa, hakurudisha matukano; alipoteswa, hakuogofya” (1 Petro 2:23).

Ungaliwauliza, naamini Menno Simons na viongozi wengine wa Wakristo wa ki-Anabatisti wangalijiunga na wanafunzi wa kwanza kwa kusema, *“Kupatanisha watu kwa Mungu na kwa wenzao ni kiini cha kazi yetu!”*

Wakristo wenye nia ya ki-Anabatisti wanaamini kwamba upatanisho ni kiini cha kazi yetu kwa njia hizi tatu:

### 1. Tusaidie watu kupatana na Mungu

Sawa na Mungu alivyochukua hatua kutupatanisha naye katika Yesu Kristo, na pia kwa binadamu wenzetu, ndivyo anavyotupeleka sisi kuchukua hatua kuleta upatanisho huo katika Yerusalemu, na Yudea, na Samaria, na hata mwisho wa nchi. Mungu ametuwekea huduma ya upatanisho.

Wakristo wa leo wenye nia ya ki-Anabatisti hutumwa kuwafanya watu kuwa wanafunzi, na kuwabatiza, na kuwafundisha mambo yote Yesu kwa jinsi alivyoishi na kufundisha. Wanataka wengine pia wamwamini Yesu, na kujiunga na jamii ya kikristo, na kutenda matendo mapya.

Kuzaliwa tena ni "mtu kujitoa maisha yake kwa kiasi anavyoweza, kwa Yesu Kristo kwa kiasi anavyomwelewa." Hapo atapewa maisha mapya. Atapewa nia mpya na Roho Mtakatifu atamwezesha kuishi kufuatana na nia hiyo mpya.

Kama mtu akipatanishwa na Mungu na maisha yake pia hubadilika. Anayemkubali Yesu, anabadilishwa mawazo yake, pamoja na urafiki wake na matendo yake. Atabadilika na kuwa mtu mpya kiakili, na kimoyo, na kimwili, na kijamii, na kisiasa. Na hivyo wamekuwa tofauti sana na dunia.

### 2. Tusaidie watu kupatana na wenzao

Kiini cha kazi yetu ni kuwapatanisha watu kwa Mungu, lakini pia kwa binadamu wenzao. Na huenda tutahitaji kutafuta chanzo cha migogoro na kuwasaidia wanaohusika kupatana. Upatanisho unahitaji kusikilizana, kutubu kweli, kusamehe bila ubinafsi, na kurudisha kilichoondolewa kwa kiasi kinachowezekana.

Msamaha huondoa kuta za vikwazo zinazotutenga na Mungu, na pia zinazotutenga na waamini wenzetu. Tunaweza kushirikiana Meza ya Bwana kwa sababu ya msamaha tuliopokea kutoka kwa Mungu na kutoka kwa wenzetu.

Sisi Wakristo inatubidi tuwe baraka kwa watu wote bila kujali walipotoka, kama ni wanaume au wanawake, au imani yao. Tunapokutana na migogoro kati ya watu au vikundi, inatubidi tuwe na "nia ya upatanisho" badala ya hukumu. Lakini hatuwezi kuongoza wengine kama sisi wenyewe hatutangulii. Tukiwashauri wengine kupatanishwa na kubadilishwa, inatubidi sisi pia kubadilishwa.

### 3. Tuwe wajumbe wa upatanisho katika dunia yetu

Upatanisho huunganisha uinjilisti na usuluhisho. Wakristo wengine wanasema kwamba uinjilisti ni kiini cha kazi yetu, na wengine wanasema ni usuluhisho, lakini tunaamini kwamba *"upatanisho ni kiini cha kazi yetu!"* Makusudi ya Mungu ni "kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake" (Wakolosai 1:20).

Wakristo wa ki-Anabatisti leo wanakataa kuingia vitani kwa sababu wanaelewa wokovu huleta mabadiliko ya maisha. Katika vita vya siku hizi, wanajeshi hujifunza uongo, na chuki, na uuaji. Watu waliobadilika hawawezi kujiunga na hayo.

Kuleta amani si kutuliza mgogoro tu. Sisi kama wanafunzi wa Yesu tuliobadilika, tunapaswa "kupiga vita" kwa nguvu zote juu ya uovu na udhalimu kuliko wengine, ila "vita" vyetu ni tofauti. Tunajiunga na Mtume Paulo alivyosema, "ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili. Maana silaha za vita vyetu si za mwili" (2 Wakorintho 10:3-4).

Historia na hali ya binadamu hutuonyesha kwamba ukatili huzidisha ukatili. Njia ya punguza ukatili na kufuata taratibu za amani na kurekebisha mambo ya udhalimu yaliyousababisha ukatili huo. Katika nyakati zote na katika hali zote tunapaswa kuiga

mfano na nia ya Yesu. Yesu alitumia maneno ya upendo na amani, badala ya bunduki na mabomu, na hivyo aliweza kuwasuluhisha na kuwavuta kuingia katika jamaa ya Mungu. Nia yetu iwe "iyo hiyo … ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu" (Wafilipi 2:5).

Suluhisho ni kazi ngumu. Inatubidi kutoa maisha yetu ili watu wa dunia yetu wapatanishwe na Mungu, na wao kwa wao, hata na maadui. Lakini hakuna furaha kubwa kuliko kuishi maisha ya amani na kuongoza wengine katika mahusiano ya amani kwa Mungu na kwa wenzao.

Kujumlisha, Wakristo wa nia ya ki-Anabatisti huamini kwamba wameitwa kwa:

1. Kupatanisha watu na Mungu.
2. Kupatanisha watu kwa binadamu wenzao.
3. Kuwa wajumbe wa upatanisho katika dunia yetu.

*Upatanisho ni kiini cha kazi yao*. Je, wewe ni Mkristo wa ki-Anabatisti?

# Neno la mwisho

Je, tunaonaje jinsi Wanabatisti wanavyelewa imani ya kikristo? Mfano wao unatufundisha nini? Zaidi ya miaka mia moja iliyopita, Professor Rufus Jones alisisitiza kwamba "kanuni kuu za nchi zetu, kama uhuru wa imani, na kutenga kanisa na serikali, na hiari ya dini, ambayo ni misingi ya demokrasi, zatoka katika imani ya Waanabatisti katika kipindi ya Matengenezo. Hao viongozi walieleza kanuni hizo kwa ujasiri na waliita makanisa kuwafuata kwa matendo yao."

Maelezo yafuatayo, je, yanaeleza jinsi unavyoelewa imani ya kikristo? Kama ndivyo, wewe ni Mkristo wa nia ya ki-Anabatisti!

**Yesu ni kiini cha imani yangu.**

_ Namtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yangu.
_ Nafafanua Maandiko kwa kuweka Kristo kwanza.
_ Nakubali ukristo wa kweli ni kumfuata Yesu katika maisha ya kila siku.

**Jamii ni kiini cha maisha yangu.**

_ Naamini kuwa msamaha ni msingi wa ushirikiano.
_ Ninasoma Maandiko pamoja na wengine ili kuelewa jinsi yanavyotuhusu leo.
_ Nakubali kwamba vikundi tunapokutana uso kwa uso ni lazima katika kanisa hai.

**Upatanisho ni kiini cha kazi yangu.**

_ Nimeitwa kupatanisha watu kwa Mungu kwa njia ya kumwamini Yesu.
_ Naamini kwamba upatanisho ni uinjilisti pamoja na usuluhisho.

_ Nakataa namna zote za udhalimu na ukatili, natafuta njia za amani badala ya vita na mashindano mengine.

# Maelezo na Maswali kwa Majadiliano
## Kanuni ya 1. Yesu ni kiini cha imani yetu

*Tumtazame Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu.*
(Waebrania 12:2)

<table>
<tr><th>Wakristo wengi wanakaza:</th><th>WaAnabatisti waongeza:</th></tr>
<tr><td>1. Kifo cha Yesu<br>Wakristo wengi wanatia nguvu hasa juu ya utakatifu wa Mungu na haja yetu ya wokovu wa kibinafsi. Wanakaza kwamba “Yesu alikuja ili afe” na hawakazi sana maisha, na mfundisho, na nguvu za Roho wa Yesu. Wanaona ukristo halisi ni msamaha.</td><td>1. Maisha ya Yesu<br>Wakristo wa ki-Anabatisti wanakubali utakatifu na neema ya msamaha ya Mungu, lakini wanakaza pia “Yesu alikuja ili aishi.” Kifo chake ilisababishwa kwa sehemu na jinsi alivyoishi. Yesu Bwana aliyefufuka anatuwezesha kumfuata katika maisha. Ukristo halisi ni kumfuata Yesu.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Je, unakubali kwamba “Ukristo halisi ni kumfuata Yesu”?</td></tr>
<tr><td>2. Kufafanua Biblia sehemu zote sawa<br>Wakristo wengi wanaangalia Maandiko, badala ya Yesu, kuwa ni mamlaka yao ya mwisho. Wanatafuta mwongozo katika Maandiko kuhusu hali za maisha yao. Maamuzi yao si lazima yalingane na mafundisho na Roho wa Yesu.</td><td>2. Kufafanua Biblia kwa kuweka Kristo mbele<br>Waanabatisti wanakubali Maandiko yote yalipumuliwa ya Mungu, lakini Yesu ndiye ufunuo kamili ya Mungu na mamlaka ya mwisho. Yesu alitimiza Agano la Kale, na ndiye kanuni kwa maisha na kwa maamuzi.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Eleza tofauti katika “Biblia sehemu zote sawa” na “Biblia ya Kristo mbele.”</td></tr>
<tr><td>3. Serikali ni mamlaka ya mwisho<br>Wakristo wengi huamini ya kwamba viongozi wa serikali watoka kwa Mungu, kwa hiyo inatupasa kuwatii hata kama wanatoa amri kinyume cha mafundisho ya Yesu au inayopinga imani.</td><td>3. Yesu ni mamlaka ya mwisho<br>Waanabatisti wanatambua kwamba serikali hutoka kwa Mungu ili kutunza maisha na taratibu katika dunia hii. Lakini amri za serikali haziwezi kuzidi neno la Yesu ambaye ni Bwana.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Ni uzito gani katika maneno, “Yesu ndiye Bwana”?</td></tr>
</table>

# Kanuni ya 2. Jamii ni kiini cha maisha yetu

*Na siku zote… wakimega mkate nyumba kwa nyumba na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote.* (Matendo 2:46-47)

| **Wakristo wengi wanakaza:** | **WaAnabatisti waongeza:** |
|---|---|
| **1. Msamaha kutoka kwa Mungu**<br>Wakristo wengi wanaweka mkazo zaidi juu ya msamaha utokao kwa Mungu kuliko msamaha kati ya binadamu. Wanaamini msamaha huleta wokovu wa mtu binafsi na maisha ya milele. | **1. Msamaha kati ya Binadamu**<br>Wakristo huhitaji kusamehewa na Mungu pamoja na kusameheana. Msamaha hujenga ushirikiano na ni njia kwa mahusiano ya amani. |
| ***Je, msamaha unaleta faida gani katika ushirikiano?*** | |
| **2. Kufafanua Maandiko binafsi**<br>Wakristo wengi wanajaribu kuelewa Maandiko kwa akili yao wenyewe na jinsi inavyohusu maisha yao. Au wengine wanategemea zaidi walimu au wachungaji wenye elimu hiyo kufafanua Maandiko. | **2. Kufafanua Maandiko katika ushirika**<br>Waanabatisti wanaamini kwamba uchunguzi wa Maandiko wa mtu binafsi utakamilishwa katika uchunguzi wa pamoja katika vikundi. Katika kikundi tunaweza kushauriana katika Roho wa Yesu. |
| ***Je, kwa njia gani mnasoma Biblia kwa pamoja katika kanisa lenu?*** | |
| **3. Kukutana katika majengo ya kanisa**<br>Wakristo wengi  hufikiri kwamba ushirika wa Wakristo katika ibada ni kanisa halisi. Mara nyingi wanapenda kuona kanisa ni jengo, au taratibu, au ibada ya Jumapili. | **3. Kukutana katika vikundi**<br>Wakristo wa ki-Anabatisti wanazoea kuona kanisa kama ni jamaii. Makanisa yaliyo hai mara nyingi yanahusiana kama vikundi vya ushirikiano, na wakisoma Biblia, na kushauriana, na kusali pamoja. |
| ***Ikiwa vikundi vidogo ni asili ya kanisa lililo hai, je, kwa njia gani vinaweza kupewa nafasi zaidi katika kanisa lako?*** | |

# Kanuni ya 3
# Upatanisho ni kiini cha kazi yetu

*Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo naye alitupa huduma ya upatanisho.* (2 Wakorintho 5:18)

| Wakristo wengi wanakaza: | WaAnabatisti waongeza: |
|---|---|
| **1. Kuhesabiwa haki kwa imani**<br>Wakristo wengi wanakaza hasa tabia ya Mungu ya utakatifu na haja yetu kuhesabiwa haki kwa imani na kwa kazi ya Kristo alivyojitoa dhabihu. Wanaona kwamba wokovu ni kusamehewa na kuwa na uhakika kwamba tutaenda mbinguni. | **1. Kubadilishwa kwa maisha**<br>Wakristo wa ki-Anabatisti hukaza tabia ya Mungu ya upendo na utunzaji. Wanatamani kubadilishwa na Roho ili kufanana na Kristo katika mawazo na matendo. Wokovu ni kupatanishwa na Mungu na kuwezeshwa kuishi kama Yesu alivyoishi katika maisha ya kila siku. |
| ***Tabia zote za Mungu ni muhimu (utakatifu, upendo). Je, ni tabia gani ni muhimu kwako?*** | |
| **2. Wokovu wa kibinafsi**<br>Wakristo wengi huelewa upatanisho kati ya mtu binafsi na Mungu. Kufanya amani na kujenga jamii ni nyongeza wala si injili halisi. | **2. Maisha ya upatanisho**<br>Waanabatisti wanaona kwamba upatanisho unahusu mtu binafsi pamoja na jamii ya watu. Uinjilisti na amani huungana katika upatanisho wa kweli. |
| ***Je, hatua za kusuluhisha katika Mathayo 18 ni zipi?*** | |
| **3. Huduma ya kijeshi**<br>Wakristo wengi wanatii mamlaka ya nchi hata kama inaamuru kinyume cha mafundisho ya Yesu na dhamira ya mtu. Wengine wanaamini kwamba kuna “ukatili unaookoa” na “vita ya haki.” Wakati serikali inapowaomba huduma ya kijeshi, wanakubali kufanya. | **3. Huduma ya badala**<br>Waanabatisti wanatii mamlaka ya dunia hapo utii kwa Kristo unapowaruhusu. Watakataa kushirikiana ukatili. Ni muhumu kurekebisha udhalimu na kupatanishwa na maadui. Wanatafuta suluhu badala ya nguvu za kijeshi. |
| ***Je, kuna matendo gani yanayojenga amani badala ya kutumia nguvu za kijeshi?*** | |

Juu ya mwandishi, Palmer Becker

Palmer Becker alisomeshwa katika vyuo vya Goshen College, na Mennonite Biblical Seminary (sasa ni Anabaptist Mennonite Biblical Seminary), Regent College, na Fuller Theological Seminary. Maisha yake yote amehudumia kanisa kama mchungaji, na mwinjilisti, mishenari, mwandishi na mwalimu. Becker ameongoza semina nyingi juu ya vikundi katika kanisa na alikuwa mkurugenzi wa idara ya masoma kwa wachungaji ya Hesston College. Karibuni amesafiri katika nchi nyingi duniani akifundisha semina. Yeye na mke wake Ardys wana watoto wane wakubwa. Becker anakaa Kitchener, Ontario, Canada.

Translated from *What is an Anabaptist Christian?* Palmer Becker, Mennonite Mission Network, Revised Edition, 2010. It is book #18 in the MissioDei series, James R. Kraybill, editor.

Translated by permission by Joseph Bontrager, 2015.